# MWONGOZO WA UTATUZI

## WA MIGOGORO YA UCHAGUZI TANZANIA

**Kimetafsiriwa na:**
Alphonce Gura (Wakili)
Francis Kajiru (Wakili)

**Kimetafsiriwa kutoka katika lugha ya Kiingereza na:**
Alphonce Gura (Wakili)
Francis Kajiru (Wakili)

**Waandishi Mwongozo katika lugha ya Kiingereza:**

Mh Jaji Mstaafu Robert Vincent Makaramba

Mh Jaji Mstaafu Dkt. Fauz Twaib

Alphonce Gura (Wakili)

Francis Kajiru (Wakili)

**Bodi ya Wahariri**

**Mwenyekiti**

Prof. Dr. Alex B. Makulilo

**Mhariri Mkuu**
Dr. Ubena John

**Wahariri:**
Dr. Eugene E. Mniwasa
Mr. Clement Mubanga
Mr. Innocent Kibadu
Ms. Beatrice Cherdiel
Mr. Mackphason Buberwa
Mr. Kaleb Gamaya

**Kimechapishwa na:**
Tanganyika Law Society
House No. 21 | Chato Street | Regent Estate
P.O.BOX 2148 | Dar es Salaam | Tanzania
**Telephone:** +255 22 277 5313 | **Fax:** +255 22 277 5314
**Email:** *info@tls.or.tz*
**Website**: *www.tls.or.tz*
**Copyright:** Tanganyika Law Society, Desemba 2020

# YALIYOMO

USULI ........................................................................................ v
SHUKRANI .................................................................................. vi

Sura ya Kwanza. ........................................................................ 1
UTANGULIZI ............................................................................... 1

Sura ya Pili .................................................................................. 4
MFUMO WA UTATUZI WA MIGOGORO YA UCHAGUZI TANZANIA: MUHTASARI ....................................................... 4

Sura ya Tatu ................................................................................ 23
UTARATIBU WA KUSIKILIZA MALALAMIKO NA UTATUAJI ................................................................................. 23

Sura ya Nne. ................................................................................ 31
MATUMIZI YA NJIA MBADALA ZA UTATUZI KUTATUA MIGOGORO YA UCHAGUZI .............................. 31

Sura ya Tano ............................................................................... 36
HITIMISHO ................................................................................. 36

# USULI

Miongoni mwa kazi za Chama cha Wanasheria ya Tanganyika (TLS) kama ilivyoainishwa katika Sheria ni kuwezesha kupatikana kwa maarifa na elimu ya sheria kwa wanachama na wanataaluma ya sheria pamoja na watu, makundi na taasisi mbalimbali. TLS kupitia Kamati ya Utafiti na Uchapishaji imetoa kipaumbele katika kuchapisha vitabu na miongozo mbalimbali ya kisheria hasa kwa ajili ya wanachama wake.

Kwa miaka mingi, TLS metoa maelfu ya machapisho ambayo inasambazwa kwa mawakili, wadau na umma kwa kusudi la kukuza ufahamu wa maarifa ya kisheria katika maeneo tofauti ya sheria. Hivi karibuni TLS imeanza kuandaa miongozo mifupi has kwa ajili yha kusaidia wanasheria wachanga waweze kufanya marejeo ya haraka. Ni imani yangu kubwa kwamba Vidokezo vya Mwongozo itakuwa moja ya njia ya kuhakikisha utoaji wa elimu ya sheria kwa wanasheria na umma kwa ujumla unakuwa endelevu.

Shukrani zangu za dhati ziende kwa wachangiaji wote, Bodi ya Wahariri na Sekretarieti kwa kazi nzuri iliyofanywa.

Prof. Dr. Alex B. Makulilo

**Mwenyekiti**

**Kamati ya Utafiti na Machapisho**

## SHUKRANI

Mwongozo huu ni juhudi ya kushirikiana na isingewezekana bila mwongozo mzuri, usimamizi na mapitio yaliyofanywa na watu kadhaa. Kwanza kabisa ni Wakili Alphonce Gura aliyeandika na kutayarisha rasimu ya kwanza ya mwongozo huu.

Kazi hii imepitiwa kwa ufasaa kabisa na Majaji Wastaafu Mhe. Robert Makaramba na Mhe. Dk Fauz Twaib. Majaji hao wawili walichangia sana mwongozo kazi kuwa kamilifu. Ukamilifu wa kazi hii pia umechangiwa kwa kiasi kikubwa na maoni yaliyotolewa na Jaji Mstaafu John Tendwa. Mapitio yamefanywa pia na Paul Anderson na Katherine Hellena kutoka IFES, ambao TLS inatoa shukrani kwao.

TLS pia inatambua usimamizi madhubuti wa kamati ya Utafiti na Machapisho chini ya uenyekiti wa Prof. Dr. Alex Makulilo, mhariri mkuu Dk. Ubena John, katibu wa kamati Wakili Beatrice Cherdiel na wajumbe wote wa kamati. Shukrani za pekeezinatolewa kwa Wakili Francis Kajiru na Wakili Pasience Mlowe, ambao walitafsiri mwongozo wa Kiingereza katika lugha ya Kiswahili.

Kazi hii pia isingewezekana bila msaada wa kifedha kutoka USAID na IFES. Waandishi wa kazi hii pia walipokea mwongozo muhimu kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa TLS, Kaleb Gamaya na mchango wa kiufundi wa katika tathmini na ufuatiliaji kutoka Seleman Pingoni. Shukrani pia zinatolewa kwa timu nzima ya Sekretarieti ya TLS kwa ushirikiano ambao umefanikisha kukamilika kwa kazi hii. Ni vigumu kutaja jina la mtu mmoja mmoja ambaye ametoa mchango katika kazi hi, lakini waandishi wa kazi hii na TLS wanatambua mchango huona kutoa shukrani za dhati.

**SEKRETARIATI YA CHAMA CHA SHERIA TANGANYIKA.**

# Sura ya Kwanza

## UTANGULIZI

Chaguzi za kidemokrasia za mara kwa mara, za kweli na ambazo ni huru na za haki, ni kielelezo cha nguvu na ukuu walinao wananchi katika kuipa Serikali msingi wa mamlaka na uhalali wa kuongoza nchi. Haki ya Wananchi ya kupiga kura na kuchaguliwa katika chaguzi za kidemokrasia zinazofanyika mara kwa mara na kwa wakati; ambazo ni za kweli, huru na haki inatambuliwa vema kama haki ya msingi katika sheria za kimataifa; na ni msingi katika kuhakikisha nchi husika inakuwa na amani, ustawi na kutoa mamlaka kwa uongozi wa kidemokrasia.

Uchaguzi ni mchakato unaoendelea wenye asili ya mzunguko ambapo mara tu uchaguzi mmoja unapokamilika na wale waliochaguliwa kuchukua viti vyao, mchakato huanza mwanzo kwa mara nyingine.

Uchaguzi uhusisha ushindani kati ya wagombea binafsi au wale wanaofadhiliwa na kuungwa mkono na vyama vya siasa vilivyosajiliwa kisheria. Kwa kuzingatia hali ya ushindani wa uchaguzi, kutokea kwa migogoro ni jambo linalotarajiwa katika mchakato wa uchaguzi. Hali hii inalazimu uwepo wa mfumo wa kusuluhisha migogoro ya uchaguzi ulio huru na wa kuaminika, usio na upendeleo, na uliojengwa katika misingi ya haki na uwazi ambao upo dhabiti kabla na hata baada ya uchaguzi. Hii sio tu italinda uadilifu na uaminifu, lakini uhalali wa uchaguzi wa kidemokrasia, na hivyo kufanya matokeo ya mwisho kukubalika na watu.

Bila shaka, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya haki ya uchaguzi na uadilifu wa uchaguzi. Migogoro ya uchaguzi huweza kutokea wakati wowote wa mzunguko wa uchaguzi. Katika mchakato wa uchaguzi mgogoro unaweza kujitokeza kwa sababu mbalimbali kwa mfano juu ya

ubadilishaji na ugawanyaji wa mipaka ya uchaguzi, usajili wa wapiga kura, uboreshaji daftari la kudumu la wapiga kura, kura za mchujo za chama na uteuzi, uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi, kupiga kura katika vituo vya kupigia kura, kuhesabu kura, kuongezea / kuhesabu kura hadi tamko la matokeo ya uchaguzi. Hivyo basi katika kila hatua mgogoro unaohusiana na uchaguzi huweza kujitokeza.

Matakwa ya haki katika chaguzi yanahitaji sana uwepo wa wadau na washiriki wenye ufahamu na taarifa kamili kuhusu mchakato wa uchaguzi na taratibu za kusuluhisha malalamiko na migogoro ambayo inaweza kutokea katika hatua tofauti za mzunguko wa uchaguzi.

## 1.1. Lengo na Madhumuni ya Mwongozo Huu.

Kuwepo kwa mfumo wa utatuzi wa malalamiko na migogoro ambayo huibuka katika mchakato wa uchaguzi ni sifa muhimu ya uchaguzi wa kidemokrasia. Mfumo kama huo unashughulikia maswala kama vile visa vya vitisho vya wapiga kura, shughuli za kampeni haramu, na ukiukaji wa taratibu za kupiga kura na kuhesabu wakati wa uchaguzi. Kwa kuwa malalamiko na mabishano yanaweza kutokea wakati wowote wa uchaguzi, na sio tu dhidi ya matokeo ya uchaguzi, kwa hivyo ni muhimu kushughulikia kasoro zozote za uchaguzi kabla ya kubadilika na kuwa migogoro mikubwa kisha kuathiri uaminifu na uadilifu wa mchakato wa uchaguzi. Ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi unahitaji suluhu na utatuzi wa haraka na kuweka vikwazo kuzuia ukiukwaji zaidi na kujenga imani dhabiti katika mchakato wa uchaguzi.

Ni kwa sababu ya lengo kuu hapo juu kwamba Mwongozo huu umeandaliwa kujenga uwezo kwa wadau na washiriki wa mchakato wa uchaguzi juu ya njia zilizopo za kutatua migogoro na suluhisho za kabla ya uchaguzi.

## 1.2. Walengwa wa Muongozo Huu.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia wadau mbali mbali wakiwemo wapiga kura, wagombea, asasi za kiraia, vyombo vya habari, waendesha mashtaka wa umma, wachunguzi, Mawakili wa Serikali, mawakili wa kujitegemea, wanasheria, mahakama na maafisa wa vyombo vya usimamizi wa uchaguzi. Mwongozo huu unawapa wadau hawa taarifa muhimu na iliyosahihi juu ya utaratibu katika mchakato wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi, kiutawala na kupitia mahakama.

Mwongozo huu pia unajumuisha majadiliano juu ya uwezekano wa kukuza utumiaji wa njia mbadala (ADR) katika kusuluhisha migogoro ya uchaguzi nchini Tanzania.

Mwongozo hata hivyo hauhusishi Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Zanzibar ina mfumo wake tofauti wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi. Zaidi ya hayo, Mwongozo haujadili utatuzi au hatua inaychukuliwa kwa makosa ya jinai katika uchaguzi. Mwongozo huu pia haujadili migogoro ya baada ya uchaguzi, kwa kuwa hii pia ina utaratibu wake tofauti hasa kwa kupitia mahakama.

# Sura ya Pili

## MFUMO WA UTATUZI WA MIGOGORO YA UCHAGUZI TANZANIA: MUHTASARI

Mfumo madhubuti wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi ni muhimu sana katika kujenga uaminifu, uadilifu na uhalali wa uchaguzi. Kwa hivyo, sheria zinazosimamia utatuzi wa migogoro na malalamiko ya uchaguzi zinapaswa kuwa sawa na kutoa suluhisho madhubuti kwa wakati unaofaa na wale wanaoshughulikia malalamiko na migogoro ya uchaguzi wanapaswa kutokuwa na upendeleo bali wawe na weledi wakutosha, ili kupata imani ya umma katika mchakato wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi.

### 2.1. Nini maana ya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi?

Hii ni mifumo rasmi na mbadala, ambayo imewekwa kusuluhisha migogoro na malalamiko ya uchaguzi. Mifumo hii inapaswa kuwa na ufanisi kushughulikia changamoto yoyote inayojitokeza wakati wowote wa mchakato wa uchaguzi.

Mifumo hii ni sehemu muhimu katika mzunguko wa uchaguzi, kwani inaathiri moja kwa moja kwa kiwango ambacho uchaguzi unachukuliwa kuwa huru na wa haki. Haihitaji kusisitizwa sana kuwa, mifumo madhubuti na inayofaa ndio msingi wa uchaguzi wa amani na wa kuaminika.

Malalamiko kabla ya uchaguzi hujumuisha yafuatayo;

- ❖ Migogoro ndani ya chama; na pia baina ya chama kimoja na chama kingine
- ❖ Malalamiko yanayohusiana na ukiukaji wa sheria na taratibu za uchaguzi na matukio ya vitendo vya rushwa katika mchakato wa uchaguzi

- ❖ Pingamizi / malalamiko yanayohusu usajili wa wapigakura
- ❖ Malalamiko / Pingamizi kwa uteuzi wa wagombea
- ❖ Malalamiko yanayohusiana na mwenendo wa wagombea wakati wa kampeni za uchaguzi
- ❖ Malalamiko yanayohusiana na ukiukaji / ukiukaji wa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi

## 2.2. Viwango vya Kimataifa vya Kutatua Migogoro ya Uchaguzi

Mfumo huu wa utatuzi ni sehemu ya haki ya uchaguzi, ambayo ni mchakato wa kuhakikisha kila hatua ya mchakato wa uchaguzi inaambatana na sheria, na inalinda haki za kimsingi za uchaguzi - haki ya kupiga kura, kuchaguliwa, kukusanyika, kuunda na kujiunga na vyama vikiwamo vyama vya siasa. Haki za kisiasa na uchaguzi huchukuliwa kama haki za kimsingi za binadamu katika sheria za kimataifa, na mifumo ya haki za uchaguzi zipo kulinda haki hizo. Kwa hivyo, utatuzi wa migogoro unawakilisha dhamana ya mwisho ya uchaguzi wa kuaminika na wa kweli.

Haki za kimsingi za uchaguzi ambazo ni sehemu ya haki za binadamu zinapatikana katika mikataba mikubwa ya kimataifa na kikanda ya haki za binadamu, matamko na kanuni. Mifano ya kawaida ni hii: Azimio la Haki za Binadamu (Ibara ya 21), Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (Ibara ya 25 (a) & (b)), Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu na Haki za Watu (Ibara ya 13), Hati ya Afrika ya Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora (Ibara ya 17 (2)), Kanuni na Miongozo ya SADC Inayosimamia Uchaguzi wa Kidemokrasia (2004), kutaja chache tu.

Azimio la Umoja wa Afrika juu ya Kanuni zinazosimamia Uchaguzi wa Kidemokrasia Barani Afrika (Sehemu ya II), zinahitaji kusisitiza kwamba ili kuhakikisha uchaguzi huru na wa haki na wa kuaminika, michakato ya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi ni pamoja na uwazi

na utatuzi kwa wakati unaofaa, wasuluhishi wasio na upendeleo ambao hutoa ufanisi na maamuzi yanayoweza kutekelezeka.

Shirika la Kimataifa la Mifumo ya Uchaguzi (IFES), kwa upande wake limekuja na kanuni saba ambazo ni sehemu muhimu ya mchakato wa uamuzi wa malalamiko, ambayo inaweza pia kuarifu mchakato wa utatuzi wa migogoro kabla ya uchaguzi. Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:

Haki ya kupata utatuzi, suluhu na kurekebisha malalamiko au migogoro inayotokea wakati wowote wa mchakato wa uchaguzi;

1) Uwepo wa Mfumo au taratibu zilizo wazi na zinazojitosheleza na kufafanua viwango vya uchaguzi na utatuzi wa migogoro itokanayo na uchaguzi;
2) Uwepo wa waamuzi wenye uwezo na weledi, na mahakama au taasisi za maamuzi zilizo huru/ hazifungamani na upande wowote
3) Uwepo wa mfumo unaoharakisha maamuzi;
4) Maamuzi sahihi ya msingi kulingana na mahitaji ya viwango vya Ushahidi katika sheria za uchaguzi
5) Upatikanaji wa suluhisho ambalo ni madhubuti;
6) Uelewa wakutosha kwa wadau mbalimbali katika utatuzi mfano wapiga kura, wapelelezi, wagombea, mahakama na vyombo vya habari

Kanuni zilizo hapo juu ni viwango vya chini kabisa vya kimataifa vya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi. Kanuni ya mwisho juu ya elimu bora ya wadau ni muhimu sana kwani inataka kuongeza na kuimarisha maarifa na uelewa wa wadau na washiriki katika mchakato wa uchaguzi juu ya taratibu katika mifumo ya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi, lengo ambalo Mwongozo huu unakusudia kufikia.

### 2.1.1. Nani anaweza kulalamika?

Kulingana na mgogoro au madai ya ukiukaji, uwezo wa kisheria wa kutoa malalamiko (msimamo wa kisheria au locus standi) hutofautiana kulingana na hatua ya mchakato wa uchaguzi na hali ya malalamiko. Hivyo basi, sheria imewapa wafuatao uwezo wa kuwasilisha malalamiko: mpiga kura halali, mgombea au mwakilishi wake aliyeidhinishwa, mawakala wa uchaguzi, vyama vya siasa, msimamizi wa uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Msajili wa Vyama vya Siasa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Swali la ni nani anaweza kulalamika au kuweka pingamizi ni muhimu, haswa ikizingatiwa kuwa asasi za kiraia (AZAKi) hazina uwezo wa kuwasilisha malalamiko au pingamizi kupitia michakato ya kiutawala ya usimamizi wa migogoro ya uchaguzi. Kwa kuongezea, sheria hailazimishi vyombo vya migogoro ya uchaguzi kutoa msaada wakati wa kujaza fomu za malalamiko au pingamizi. Hii inamaanisha kuwa ni hiari ya maafisa husika kumsaidia mlalamikaji na kukubali malalamiko licha ya makosa ya kiutaratibu au kuyatupilia mbali kwa makosa ya kiutaratibu. Hivyo basi, AZAKi zinaweza kuwa nafasi muhimu katika kuwaongoza walalamikaji au wapingaji kuhusu utaratibu sahihi na kamilifu wa kufuata kisheria ili kuwasilisha malalamiko au pingamizi.

Mlalamikaji au mpingaji anapaswa kuwa na nia ya kuhakikisha kuwa dai lililoandikwa linajumuisha maelezo yanayohusiana na ukiukwaji unaodaiwa, kama vile tarehe, saa, mahali na habari juu ya mtu au taasisi ambayo madai au pingamizi limewasilishwa. Maelezo ya mawasiliano ya mtu anayeweka pingamizi au dai inapaswa kujumuishwa pia.

Ingawa sheria imeacha mamlaka ya kutoa uamuzi kwa vyombo vya kusuluhisha migogoro ya uchaguzi katika mambo mengi, bado ni busara kwa mdai au mpingaji kuomba adhabu ambayo

anahitaji itolewe au kueleza nini mamlaka imfanyie katika madai au pingamizi la maandishi. Pamoja na hayo, ushahidi kamili unapaswa kuwasilishwa kuunga mkono madai hayo.

### 2.1.2. Malalamiko yanaweza kuletwa dhidi ya nani?

Sheria imeweka njia za kufungua malalamiko dhidi ya Tume, Wasimamizi wa Uchaguzi, na Serikali. Walakini, Tume ina kinga ya kikatiba kwa mambo yaliyofanywa kulingana na mamlaka yake ya kikatiba na kisheria. Hata hivyo, hii haizuii kuwasilisha malalamiko dhidi ya serikali kortini kwa matumizi mabaya ya mamlaka na viongozi wa serikali; kutumia rasilimali za serikali kufanya kampeni; kuzuia au kuvuruga hafla au sughuli za umma zilizofanyika kwa mujibu wa mpango wa kampeni ulioratibiwa, au kuruhusu vyombo vya usalama kukandamiza vyama vya siasa, wagombea au wafuasi.

Sheria pia inakataza maafisa wa NEC au wasimamizi kujihusisha na vitendo vya rushwa, vitendo vingine haramu au kukiuka sheria na kanuni za uchaguzi; hivyo malalamiko yanaweza kuwasilishwa dhidi ya maafisa hao wa serikali kutokana na sababu hizi. Kwa kuongezea, Kamati za Maadili ambazo zinajumuisha watu wanne wamepewa jukumu la kusikiliza na kuamua juu ya malalamiko dhidi ya viongozi wa NEC na wasimamizi lakini tu kuhusiana na kampeni za uchaguzi. Katika Uchaguzi Mkuu uliomalizika wa 2020, palikuwapo na malalamiko mengi dhidi ya wagombea juu ya ukiukaji wa Maadili ya uchaguzi.

### 2.1.2. Vigezo vya pingamizi/malalamiko halali.

Sheria inahitaji uwepo wa pingamizi/lalamiko halali. Sharti hili hata hivyo, linatofautiana kulingana na hatua ambayo malalamiko au pingamizi linaletwa. Walakini, mtu anayeleta malalamiko au pingamizi anahitaji kuzingatia matakwa katika kujaza fomu za kuweka pingamizi au lalamiko kulingana na sheria, kanuni na miongozo ya uchaguzi. Ni muhimu pia kutambua chombo sahihi

chenye mamlaka kisheria ya kusilikiza lalamiko ama mgogoro husika.

### 2.1.3. Aina ya ushahidi unaohitajika kuthibitisha shtaka.

Aina tofauti za ushahidi unweza kuwasilishwa kulingana na uhalisia wa lalamiko/pingamiz husika. Mfano, nakala ya majina/orodha ya wapiga kura, nakala ya hati ya uteuzi wa mgombea, matamko na taarifa zozote za umma kutoka kwa wagombea, hati za viapo kutoka kwa mashahidi wenye ufahamu wa kibinafsi wa tukio fulani, ushuhuda wa wataalam, nakala ya hukumu au maagizo ya mahakama, taarifa za kifedha za benki, ripoti za fedha za kampeni, makaratasi ya kupigia kura, nakala za matokeo; matangazo au mabango ya kampeni, mahojiano yaliyorekodiwa kupitia vyombo vya habari, data zaki elektroniki na picha, audio au video, masanduku ya kura, karatasi za kupigia kura au ripoti za waangalizi wa vituo vya kupigia kura siku ya uchaguzi au ripoti za wasimamizi wa uchaguzi zinaweza kutolewa kama ushahidi na zingine ambazo hazijaorodheshwa hapa zinaweza kuwasilishwa kama ushahidi.

### 2.1.4. Wajibu wa kuthibitisha madai.

Mlalamikaji au mpingaji ana jukumu la kuthibitisha madai yake kwa ushahidi madhubuti na unaojitosheleza. Hivyo basi ni muhimu sana kwa mlalamikaji kuwa na ushahidi unaojitosheleza ili kuweza kutetea msingi wa malalamiko/pingamizi lake dhidi ya mgombea mwingine. Kwa baadhi ya madai, taasisi za uchaguzi zinaweza kukusanya ushahidi kwa kutumia uchunguzi wao kwa lengo la kuhakikisha malalamiko yanaamuliwa kwa haki. Mfano kamati ya maadili inaweza kufanya upelelezi wakati wa kampeni.

Inafaa kuzingatia hapa kwamba mchakato wa utatuzi kama unavyotolewa katika sheria za uchaguzi za Tanzania, ukizangatia viwango vya kimataifa vya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi, si wa usuluhishi na upatanishi bali umejikita katika kutoa maamuzi

yanayowafunga pande mbili. Sheria za uchaguzi za Tanzania zimeundwa zaidi kutoa nguvu kwa chombo cha kusuluhisha migogoro kutoa uamuzi juu ya jambo linalobishaniwa. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kuwa viwango vya ushaidi vinavyohitajika sio vya juu sana hasa kwa mamlaka za kiutawala. Mamlaka hizi zinahitaji uthibitisho tu kwasababu hazifungwi na kanuni za Ushahidi zitumikazo mahakamani.

### 2.1.5. Hukumu/maamuzi/adhabu

Vyombo vya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi vina mamlaka ya kutoa aina tofauti za adhabu na vizuizi mara tu madai hayo yatakapothibitishwa, kama ifuatavyo:

- Kurekebishwa kwa daftari la wapiga kura (kuhifadhi au kufuta majina) ikiwa malalamiko au pingamizi linahusiana na usajili wa wapiga kura au kutolewa kwa kitambulisho cha mpiga kura au kusalimishwa kwa kadi ya mpiga kura;
- Fidia ya fedha;
- Malipo ya faini;
- Onyo au karipio kwa wagombea na watu binafsi;
- Kuamuru mlalamkiwa kusahihisha makosa au kubadilika;
- Tangazo la umma na onyo kwa umma kwa vyama vya siasa ambalo linaweza kuwa la wazi;
- Kusimamishwa, kutolewa au kushitakiwa kwa kosa la jinai dhidi ya watu binafsi na vyama vya siasa;
- Kuzuia chama cha siasa au mgombea kuendelea na kampeni;
- Kuenguliwa chama cha siasa au mgombea katika uchaguzi;
- Kufungwa kwamgombeai haswa kwa makosa yanayohusiana na gharama za uchaguzi
- Kupewa onyo la maandishi

- Vitendo vya kurekebisha (kwa mfano, kumtaka mkiukaji wa sheria kutoa mabango ya uchaguzi katika majengo ya uma, waombe mawakala kuondoka katika vituo vya kupigia kura, kupendekeza mafunzo mengine ya ziada na kuchukua hatua zinazohitajika)
- Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya afisa wa tume au msimamizi (mfano kufukuzwa au kusimamishwa) au kufahamisha mamlaka zinazohusika juu ya ukiukaji wa maafisa wake
- Kusimamishwa au kufutwa kwa chama;
- Kufutwa kwa idhini ya waangalizi wa uchaguzi;
- Kufutwa kwa kura, au uchaguzi, kuahirisha au kusimamisha upigaji kura
- Kumfuta mgombea
- Kufutwa kwa idhini ya wakala wa mgombea; na
- Kumtangaza mgombea kama kashindwa au kashinda.

Ni muhimu kutambua kwamba ikiwa madai hayo yamethibitishwa kuwa si ya kweli na hayana mashiko mpingaji au mlalamikaji anaweza kukabiliwa na adhabu. Kwa mfano, upingaji dhidi ya usajili wa wapiga kura, ikiwa utafanywa bila sababu ya msingi, atatakiwa kulipa fidia. Pia fidia hizi zinazoamuliwa na Kamati za maadili zinaweza pia kuwapata waliowasilisha malalamiko juu ya kampeni zisizo za haki bila sababu za msingi. Adhabu zinazotolewa zinapaswa kulingana na ukali wa ukiukaji wa sheria au utaratibu husika.

Vyombo vya maamuzi pia vinaweza kufutilia mbali malalamiko kutokana na ukosefu wa ushahidi wa kutosha.

### 2.1.6. Muda wa Utatuzi, ukamilifu/utoshelevu na uwiano wa hukumu/maamuzi.

Wakati wa kuchunguza kama mgogoro umeamuliwa kikamilifu, kuna umuhimu kubainisha ikiwa sababu za kila lalamiko limeelezewa kikamilifu, kuna muongozo wa kutosha wa kisheria unaotoa njia za kushughulikia malalamiko haya, kuangalia kama aliyeshindwa katika shauri husika anaweza kukata rufaa, na kama maamuzi yamefikiwa katika muda unaotakiwa na adhabu zilizopo katika kila kosa.

Kwenye baadhi ya taratibu za uchaguzi, sababu zilizotajwa hapo juu huzingatiwa kwa umakini, mfano kwenye malalamiko dhidi ya usajili wa wapiga kura, uteuzi wa mgombea, kampeni, upigaji na uhesabuji wa kura na utangazaji waa matokeo.

Hata hivyo, baadhi ya michakato au hatua nyingine za uchaguzi sheria haijaweka wazi na kwa ukamilifu jinsi ya kusikiliza malalamiko haya na adhabu husika. Hatua hizi zinajumisha migogoro ya ndani ya chama juu ya uteuzi wa wagombea, migogoro baina ya vyama inayohusiana na mchakato wa uchaguzi, kukataa kuidhinisha waangalizi au kutostahiki kwa waangalizi, na malalamiko juu ya ufikiwaji wa vyombo vya habari, waangalizi na mawakala wa chama. Taratibu hizi zinaweza kuwekwa ndani ya mfumo uliopo wa kanuni zinazosimamia uchaguzi.

### 2.1.7. Tofauti ya Mamlaka kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Kamati ya Maadili na mamlaka ya utekelezaji.

Baadhi ya ukiukaji unaweza kuhusishwa na mamlaka ya NEC, Kamati za Maadili na vile vile mamlaka ya kutekeleza sheria ya jinai kama vile Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Mifano ya ukiukaji kama huu ni pamoja na vitendo visivyo vya haki kama rushwa, kushawishi wapiga kura na wateule wakati wa kampeni. Makosa mengine ya uchaguzi ni

pamoja na kupiga kura nyingi (kuiga) siku ya uchaguzi, kununua kura (rushwa) au vitisho kwa wapiga kura kumpigia mgombea fulani (tishio au ushawishi usiofaa). Adhabu/hukumu na ushahidi wa kudhibitisha madai hayo hutofautiana kutoka kwa kosa moja hadi lingine.

NEC au Kamati za maadili zinaweza kushughulikia ukiukaji wa sheria za uchaguzi ambazo ni za kijinai kiutawala kwa kutoa adhabu za kiutawala au inaweza pia kuitaka mamlaka ya mashtaka kupeleka mashtaka ya jinai mahakamani. Inashauriwa hatua za kiutawala zizingatiwe zaidi sababu ni rahisi na haraka tofauti na jinai.

Sheria inawapa TAKUKURU uwezo wa kuchunguza na kushtaki malalamiko yanayohusiana na gharama za uchaguzi na viashiria vya rushwa katika hatua yoyote ya mchakato wa uchaguzi. Tatizo la kisheria ni kuainisha vitendo vya rushwa na haramu katika sheria za uchaguzi kama “mazoea” tu na sio uhalifu wa kiuchumi na hivyo kuifanya iwe ngumu sana kwa TAKUKURU kuwashuhulikia wanaokiuka sheria ya uhalifu wa kiuchumi. Kwa hali yoyote, hakuna mahitaji ya wazi katika sheria ya uchaguzi kwa NEC, wasimamizi au kamati za maadili kupeleka kesi kwa TAKUKURU au Polisi kwa uchunguzi na mashtaka katika korti za jinai.

### 2.1.8. Uwazi katika mwenendo wa uchunguzi na usikilizaji wa malalamiko/migogoro.

Sheria inavitaka vyombo vya maamuzi kusikiliza mashauri huku wahusika wakiwepo pale tu kwenye ulazima. Kwa hivyo NEC, wasimamizi na kamati ya maadili zinaweza kupanga usikilizwaji ili kuruhusu vyama kuwasilisha hoja zao, ushahidi na utetezi. Kumbuka inapaswa kuzingatiwa kuwa vyombo hivi vya kiutawala havilazimishwi chini ya sheria kufanya vikao vya mashauri na kufanya maamuzi wakati upande mmoja au pande zote mbili zipo. Vivyo hivyo, hakuna sharti chini ya sheria kwa vikao vya usikilizaji

kutolewa kwa umma. Pia, hua vikao haviko wazi kwa umma kama ilivyoainishwa katika ripoti za uchunguzi wa chaguzi zilizopita. Kwa kuongezea, hakuna kifungu katika sheria kinachoruhusu wapiga kura na waangalizi wa uchaguzi kuhudhuria vikao hivi.

Isipokuwa kwa mahakama pekee ambapo mashauri ya uchaguzi husikiliwa kwenye mahakama ya wazi ambapo mahali na wakati vinajulikana kisheria, vyombo vingine ya utatuzi wa malalamiko/ migogoro ya uchaguzi havina mwongozo wa kisheria kuhusu wakati na mahali pa kusilikiliza mashauri. Kwa hivyo, inadhibitishwa kuwa sio lazima kwa vyombo vya migogoro ya utatuzi kufanya vikao vya usikilizaji katika eneo ambalo madai ya ukiukaji au malalamiko yalitokea. Haihitaji kutiliwa mkazo kuwa kusikilizwa lalamiko katika jimbo husika kunatoa ufikiaji rahisi wa haki na kupunguza mzigo kwa walalamikaji, wahojiwa na mashahidi wanaopaswa kusafiri kwenda mahali pa kusikilizwa kutafuta haki ya uchaguzi.

Msisitizo unaweza kuwekwa hapa kwamba ni muhimu vyombo hizi vya utatuzi viendeshe mashauri katika maeneo husika kwasababu ya wepesi wa kufikiwa na walalamikaji, walalamikiwa na mashaidi vile vile jambo ambalo ni muhimu katika upatikanaji wa haki. Kwa mantiki hii ni vema kufikiria jisni ya kuboresha kanuni za utatuzi wa migogoro kiutawala ili kufanya mikutano ya kiutawala iwe wazi na hivyo kuinua imani na uaminifu wa pande zinazohusika na kufuata viwango vya kimataifa vya utatuzi wa migogoro.

### 2.1.9. Utoaji, Uchapishaji na Utangazaji wa Maamuzi

Sheria imetoa muda wa kutolewa kwa maamuzi na Kamati za NEC, maadili na wasimamizi kwenye baadhi ya malalamiko, japo si yote. Katika matukio mengine, sheria imevitaka vyombo kutoa taarifa ya kutosha (notisi) kwa wahusika juu ya hukumu itolewayo au pindi maamuzi yanapokuwa yamefikiwa. Hata hivyo sheria haiitaji vyombo hivi kutoa maamuzi ya maandishi na ya kina yakisema wazi

sababu ya kufikia uamuzi huo. Sheria pia haiitaji Kamati ya NEC / RO / Maadili kuweka hadharani maamuzi yaliyofikiwa na haiitaji vyombo kutoa nakala za uamuzi kwa wadau.

Walakini, kwakuwa vyombo hivi ni vya kiutawala kwa hiyo vinafungwa na kanuni za haki ya asili ambayo inahitaji ufafanuzi wa kina wa sababu za maamuzi. Ni kwa sababu hiyo sheria za uchaguzi zimetoa ufikiaji wa kutosha kwa uhakiki wa kimahakama (judicial review) ikiwa kanuni hizo zinazingatiwa. Hivyo yeyote asiyeridhishwa na maamuzi fulani anaweza kwenda mahakamani.

## 2.3. Mfumo wa Sheria wa Utatuzi wa migogoro ya uchaguzi nchini Tanzania.

Mfumo wa sheria za utatuzi wa migogoro ya uchaguzi unajumuisha sheria za haki ya msingi na sheria za kiutaratibu kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini. Kutokana na Tanzania kuwa na mamlaka ya nchi huru ya Jamhuri ya muungano, basi kuna sheria za uchaguzi ambazo zinatumika kwa "Muungano" wote kama vile Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi, kuna zingine ambazo zinatumika tu katika sehemu husika za "Muungano" kama sheria za uchaguzi zinazosimamia uchaguzi wa mamlaka za mitaa.

### 2.3.1. Mfumo wa Sheria za Utatuzi wa Migogoro ya Uchaguzi Tanzania:

| Masharti ya Katiba | Sheria ya Kitaifa | | Sheria za Mamlaka za Mitaa | |
|---|---|---|---|---|
| | Sheria kuu | Sheria tanzu | Sheria kuu | Sheria tanzu |
| Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 | Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343 | Kanuni za Uchaguzi wa Kitaifa (Uchaguzi wa Rais na Wabunge) gazeti la Serikali namba 402 ya 2020 | Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa [Uchaguzi] Na. 292 iliyofanyiwa marekebisho 2015 | Kanuni za Mamlaka za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani), gazeti la serikali namba 401 ya 2020 |
| | | Kanuni za Uchaguzi wa Kitaifa (Mashauri ya Uchaguzi), 2020 gazeti la serikali namba 782 iliyochapishwa mnamo 18/09/2020] | Vifungu kadhaa katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Na. 7 ya 1982 [Sura. 287 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2002] na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Na. 8 ya 1982 [Sura. 288 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2002] | Kanuni za Mamlaka za Mitaa (Mashauri ya Uchaguzi), 2010 Gazeti la serikali namba 783 iliyochapishwa mnamo 18/09/2020] |
| | Sheria ya Vyama vya Siasa | | | |

### 2.3.2. Mfumo wa Sheria za Utatuzi wa Migogoro ya Uchaguzi Zanzibar.

- Katiba ya Zanzibar ya 1984
- Sheria ya Uchaguzi, Sheria ya 2017 Na. 4 ya 2018, ilifuta na kuchukua nafasi ya Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya 1984
- Sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya 2017, Sheria Namba 1 ya 2017
- Sheria ya Kura ya Maoni, 2010, Sheria Na. 6 ya 2010
- Sheria ya Serikali za Mitaa ya Zanzibar, Sheria ya 1984 Na. 7 ya 2014

## 2.4. Mfumo wa taasisi katika utatuzi wa migogoro ya kiuchaguzi.

Ingawa kikatiba ni "Mamlaka huru ya Serikali ya Muungano", Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina pande mbili katika mifumo ya sheria na mahakama. Usimamizi wa uchaguzi, utatuzi wa migogoro ya uchaguzi na mashauri ya uchaguzi pia ni sehemu katika mfumo huu wa pande mbili. Tofauti na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inayosimamia kwa jumla uchaguzi wa urais na wabunge na uchaguzi wa madiwani Tanzania Bara, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) ina mamlaka ya jumla juu ya uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na uchaguzi wa serikali za mitaa katika Tanzania Zanzibar.

Mamlaka ya kutatua migogoro ya uchaguzi nchini Tanzania iko katika taasisi kadhaa. Kimsingi, migogoro na rufaa zinazotokea wakati wa hatua za uchaguzi zinaweza kushughulikiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kamati za maadili, wasimamizi wa Uchaguzi, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

Migogoro ya uchaguzi inaweza kuwa ya kiutawala, kimadai na kijinai. Hii inamaanisha kuwa njia za kusuluhisha migogoro ya

uchaguzi lazima ziwe za kurekebisha na za kuadhibu; kurekebisha kwasababu hubatilisha au kurekebisha makosa; na kutegemea na sula husika, pia kulinda au kudumisha haki za kikatiba katika uchaguzi; na tatu ni ni adhabu kwa sababu huadhibu mtu au taasisi inavyovunja utaratibu wa kisheria wa uchaguzi.

### 2.4.1. Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ni zao la Katiba. Kwa mujibu wa kifungu cha 74 (12) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, mahakama imezuiliwa kuingilia "chochote kinachofanywa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii." Kifungu cha 74 (14) cha Katiba kinasema kuwa "watu wanaohusika na mwenendo wa uchaguzi" wamekatazwa kujiunga na chama chochote cha kisiasa, isipokuwa tu kwamba kila mmoja atakuwa na haki ya kupiga kura. Tume ya taifa ya uchaguzi ndiyo taasisi pekee nchini iliyo na jukumu la kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Kulingana na mgogoro au madai ya ukiukaji, msimamo wa kisheria unatofautiana: Mpiga kura, mgombea au mwakilishi wake aliyeidhinishwa, mawakala wa uchaguzi, vyama vya siasa, msimamizi, NEC yenyewe, Msajili wa vyama vya Siasa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wana haki ya kufungua kesi. Msimamo wa kisheria umewekwa kwenye jedwali Na 1. Lililoambatinishwa katika mwongozo huu.

Sheria pia imeweka njia za kufungua malalamiko dhidi ya NEC yenyewe, wasimamizi na serikali.

### 2.4.2. Kamati ya Maadili

Kamati za maadili zimeainishwa katika Maadili ya Uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani wa Juni 2020 na imeundwa kusaidia kutatua migogoro inayotokea wakati wa kampeni. Kamati zinaundwa na maafisa wa tume, wawakilishi kutoka kwa serikali na vyama vya

siasa na hufanya kazi kwa kujitegemea bila kuingiliwa na tume.

Kamati za maadili zimepewa mamlaka ya kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa kanuni za maadili. Kamati za maadili zimeanzishwa katika ngazi ya kata, jimbo na kitaifa. Kamati ya rufaa pia imeundwa katika ngazi ya kitaifa. Kamati ya rufaa inasikiliza rufaa kutoka kamati ya kitaifa ya maadili. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwenye ngazi yoyote kati ya hizi (isipokuwa moja kwa moja kwa kamati ya rufaa) na ikiwa bado hajaridhika na matokeo, suala hilo linaweza kukatiwa rufaa mahakamani.

Kiufupi rufaa ziko katika ngazi mbili. Ngazi ya kwanza inahitaji ukamilifu wa rufaa katika ngazi zote za juu za kamati za maadili hadi kufikia kamati ya rufaa. Pili ni Mahakama Kuu kusikilia rufaa ya mashauri ya uchaguzi yanayotokana na maamuzi ya kamati ya rufaa. Inapaswa kuzingatiwa kuwa madaraka ya kamati za maadili ni kwa wakati wa kampeni tu.

Maadili ya Uchaguzi yametolewa chini ya kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi [Sura. 343 toleo lililorekebishwa 2015], ambayo ilifanyiwa marekebisho na Sheria Namba 7 ya 2010 [kifungu cha 26]. Kifungu cha 124A ni sehemu mpya iliyoletwa katika Sheria ya Kitaifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi (Marekebisho anuwai), Na. 7 ya 2010. Marekebisho hayo yameingizwa kama sehemu ya 124A - Kanuni za Maadili ya Uchaguzi - katika Sura ya IX inayoitwa "Fedha na Utoaji wa anuwai" Inasimamia mwenendo wa maadili ya vyama vya siasa, Serikali na Tume (NEC) na inawafunga vyama waliosaini.

Maadili ya uchaguzi yaliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) yatatumika kwa-

a. Kila chama cha siasa

b. Kila mgombea wa uchaguzi

c. Serikali

d. Tume

Mgombea anayependekezwa anahitajika kujiandikisha kwenye Kanuni za Maadili ya Uchaguzi kwa kutumia Fomu Namba 10 kama ilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Kanuni hizi.

Mgombea anayependekezwa wa uchaguzi anahitajika kupata Fomu Namba 10 kutoka kwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi pamoja na fomu za uteuzi kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 24.

Kifungu cha 124A cha Sheria na Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ziliweka sharti la mapema la kuripoti malalamiko yoyote yanayotokea katika mchakato wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na wakati wa kampeni za uchaguzi kwa Kamati ya Maadili.

Kesi ya DANIEL NSANZUGWANKO VS. WAKILI Mkuu, rufaa ya kiraia Namba 106 ya 2012 (haijaripotiwa) imeelezea suala la kutopeleka lalamiko katika kamati ya maadili chini ya kifungu 124A cha Sheria ya Kitaifa ya Uchaguzi, kinamzuia mlalamikaji kuwasilisha ombi la kuzuia uchaguzi.

Baada ya kusikia ombi la uchaguzi, Mahakama Kuu ilihitimisha kuwa kutowasilisha malalamiko kwa Kamati ya maadili hakumzuii mwombaji kufungua ombi la kupinga matokeo ya uchaguzi. Katika rufaa, Mahakama ya Rufaa ilishikilia kwamba;

> "... mrufani ambaye alikuwa amesaini Kanuni za Maadili za Uchaguzi alilazimishwa na Kanuni hiyo kuripoti malalamiko hayo. Tunakubaliana na Jaji msomi wa Mahakama Kuu kwamba kushindwa kupeleka malalamiko kwenye Kanuni za Maadili ya Uchaguzi hakumzuii mwombaji huyo kuwasilisha ombi lakini inaongeza nguvu kwenye kesi yake kwani kiwango cha uthibitisho katika maombi ya uchaguzi ni "ushahidi bila shaka yoyote"

### 2.4.3. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa

Sheria ya Marekebisho ya Vyama vya siasa, Sheria Namba 1 ya 2019, ilifanya marekebisho makubwa katika Sheria ya vyama vya siasa [Sura ya 258 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2019] katika kifungu cha 4 kwa kuongeza kifungu cha 5 juu ya majukumu ya Msajili wa vyama vya siasa, kujumuisha (b) kufuatilia uchaguzi wa ndani ya chama na mchakato wa uteuzi.

Sehemu ya 6C ya sheria iliyorekebishwa pia inatoa sifa za kuwa mwanachama wa chama cha siasa na inakataza mtu kuwa mwanachama wa chama zaidi ya kimoja cha siasa.

Sehemu ya 11A ya sheria iliyobadilishwa sasa inaruhusu kuunda umoja wa vyama vya siasa vilivyosajiliwa kikamilifu kwa makubaliano kabla au baada ya uchaguzi mkuu.

### 2.4.4. Baraza la Vyama vya Siasa

Sheria ya vyama vya siasa haitengenezi taasisi huru na isiyo na upendeleo kwa kusuluhisha migogoro ya vyama. Sheria hiyo inataja tu kuanzishwa kwa Baraza la vyama vya siasa chini ya kifungu cha 21B (1) cha Sheria ya vyama vya siasa, ambayo uanachama wake umetolewa chini ya kifungu cha 21B (2) "sio zaidi ya viongozi wawili wa kitaifa wa kila chama kilichosajiliwa kikamilifu." Baraza hili lina jukumu la kushauri tu kwa kazi za Msajili wa vyama vya siasa, serikali na vyama vya siasa. Kwa hivyo, migogoro mingi ya ndani ya chama husikilizwa mahakamani (pale mwanachama anapovuliwa uanachama).

Suala linalosumbua ni, je hali ya kisiasa nchini Tanzania imeimarika ili kuanzishwa kwa Mahakama huru ya usuluhishi wa migogoro ya vyama vya siasa ili kushughulikia migogoro ya ndani ya chama na kati ya vyama vya kisiasa kama ilivyo katika Kenya ambapo Mahakama hiyo ipo?

Nchini Kenya, sheria ya vyama vya siasa ilianzisha mahakama ya migogoro ya vyama vya siasa, ambayo imepewa mamlaka ya kuamua migogoro kati ya: kwanza, wanachama wa chama cha siasa; pili, wanachama wa chama cha siasa na chama cha siasa; tatu, vyama vya siasa; nne, mgombea huru na chama cha siasa; na tano washirika wa muungano. Kama sharti la kuwezesha mamlaka ya mahakama hii, vyama lazima vitumie kwanza njia za ndani za utatuzi wa migogoro ya vyama vyao vya kisiasa kabla ya kupelekwa kwa mahakama hiyo. Chini ya sheria hiyo, mahakama hiyo pia inasikiliza rufaa ya maamuzi ya msajili.

# Sura ya Tatu

## UTARATIBU WA KUSIKILIZA MALALAMIKO NA UTATUAJI

Mfumo wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi nchini Tanzania unashughulikia kwa kina migogoro na malalamiko kwa kila hatua ya mzunguko wa uchaguzi. Wakati wa kuzingatia utoshelevu na muda wa kushughulikia malalamiko ni muhimu kubainisha ikiwa sababu za kila malalamiko zimeelezewa / kuelezewa wazi, kuna namna ya wazi kwa mamlaka ya kushughulikia migogoro, ikiwa uamuzi unaweza kukatiwa rufaa, ikiwa kuna muda maalum hadi kufikia uamuzi na suluhisho zinazopatikana kwa kila madai.

### 3.1. Malalamiko ya Usajili wa Wapiga Kura

Vifungu vya 24 na 25 vya sura ya 343 vinatoa utaratibu wa kutoa pingamizi katika hatua ya usajili wa wapiga kura. Kifungu hicho kinataja aina ya watu wanaoweza kutoa pingamizi, ambao ni; mkurugenzi wa uchaguzi; afisa usajili na mtu mwingine yeyote ambaye jina lake linaonekana katika daftari la wapiga kura la muda. Pia pingamizi zinahusiana na madai kwamba mpiga kura aliyesajiliwa hakustahili, hana sifa tena au amekufa.

Kifungu cha 26 cha sura 343 hutoa mamlaka ya uchunguzi na uamuzi kwa afisa wa usajili. Kifungu hiki ki wazi kwamba ikitokea pingamizi, afisa wa usajili lazima afanye uchunguzi na mpingaji anatakiwa kutoa uthibitisho wa kwanza wa madai hayo. Ikiwa pingamizi halikuwa na sababu za msingi, afisa wa usajili anaweza kuagiza fidia kwa mtu ambaye pingamizi hilo limetolewa na agizo

hilo ni sawa na amri ya mahakama ya wilaya juu ya urudishaji wa fedha [kifungu cha 26 (6) cha sura. 343].

Sehemu ya 27 ya sura 343 inatoa rufaa kwa hakimu wa wilaya. Inasema kwamba ikiwa mpingaji haridhiki na uamuzi wa afisa usajili, anaweza kukata rufaa kwa mahakama ya wilaya ndani ya siku saba za uamuzi [kifungu cha 27 (1) cha sura. 343]. Mahakama ya wilaya inalazimika kuamua rufaa hiyo ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha rufaa [kifungu cha 27 (2) cha sura. 343].

Sheria hiyo inaweka bayana kwamba uamuzi wa mahakama ya wilaya "utakuwa wa mwisho na hautapingwa katika mahakama yoyote" [kifungu cha 28 (2) cha sura. 343].

Sheria inaamuru hakimu wa wilaya kupeleka taarifa iliyo na majina ambayo ameamua yafutwe kwenye daftari la muda la wapiga kura na taarifa ya jina la mtu yeyote ambaye kadi ya mpiga kura itapewa na kumjulisha mkurugenzi wa uchaguzi juu ya matokeo ya rufaa [kifungu cha 28 (3) cha sura. 343],

Pale ambapo rufaa imetupiliwa hakuna mtu yeyote katika rufaa atakayepata gharama yoyote au fidia [kifungu cha 28 (5) cha sura. 343]. Shahidi anaweza kuitwa na kuapishwa wakati wa kusikilizwa kwa rufaa kama vile wakati wa kesi ya mahakama ya wilaya katika utekelezaji wa mamlaka yake ya jinai [kifungu cha 28 (7) sura. 343]. Hakimu wa wilaya ana mamlaka ya kuamua juu ya utaratibu wa rufaa za kusikiliza.

Ikiwa imeridhisha kwamba rufaa mbili au zaidi zinahusisha swali moja, hakimu wa wilaya anaweza kutamka kuwa uamuzi uliotolewa katika rufaa iliyosikilizwa hapo awali utakuwa wa pande zote kwa rufaa nyingine kama atakavyosema [kifungu cha 28 (9) ya sura. 343].

## 3.2. Malalamiko ya Uteuzi wa Wagombea

### 3.2.1. Pingamizi la Uteuzi wa Mgombea Urais na Makamu wa Rais

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea urais na mgombea wa makamu wa rais zimetolewa chini ya kanuni ya 28 ya gazeti la serikali namba 401 na Kanuni ya 31 ya gazeti la serikali namba 402 na Kanuni ya 29 ya gazeti la serikali namba 401. Rufaa zinaweza kuchukuliwa chini ya kanuni ya 32 ya gazeti la serikali namba 402 na Kanuni ya 30 ya gazeti la serikali namba 401.

Pingamizi na maamuzi kuhusu uhalali wa fomu ya uteuzi wa urais - zimetolewa katika sehemu ya 40 Sura ya 343 na Kanuni ya 39 ya gazeti la serikali namba 402.

### 3.2.1. Sababu za Kupinga Uhalali wa Fomu ya Uteuzi.

Kifungu cha 40(1) cha Sura ya 343 kinatoa sababu za kupinga uhalali wa fomu ya uteuzi, ambayo inaweza kufanywa kwa fomu ya uteuzi tu kwa sababu zote au kwa sababu zifuatazo:

(a) Kwamba maelezo yaliyotolewa kwa mgombea hayatoshi kumtambua;

(b) Kwamba fomu ya uteuzi haizingatii au haikutolewa kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii;

(c) Kwamba ni dhahiri kutokana na fomu ya uteuzi kwamba mgombea hana sifa ya kugombea;

(d) Kwamba mahitaji ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 38 hayajazingatiwa; au

(e) Ikiwa mahitaji ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi hayajazingatiwa

### 3.2.2. Nani anaweza kupinga?

Pingamizi linaweza kutolewa na mgombea mwingine katika jimbo, mkurugenzi wa uchaguzi, msajili wa vyama vya siasa au msimamizi wa uchaguzi kwa hoja yake mwenyewe au mwanasheria mkuu wa

serikali, kwa maandishi na kutiwa saini na mpingaji na kubainisha sababu za pingamizi [kifungu 40(3) ya sura. 343].

Kanuni ya 30(1) ya tangazo la serikali namba 402, inasema kwamba kulingana na masharti ya sheria, mkurugenzi wa uchaguzi, msajili wa vyama vya siasa, msimamizi wa uchaguzi, mwanasheria mkuu wa serikali au mgombea ubunge anaweza kuweka pingamizi kwa uteuzi wa mgombea yeyote wa ubunge.

(2) Mtu anayetaka kupinga uteuzi wa mgombea chini ya kanuni ndogo ya (1) atawasilisha pingamizi lake kwa msimamizi wa uchaguzi wa jimbo baada ya kuonyesha fomu za uteuzi lakini sio zaidi ya saa kumi alasiri ya siku inayofuata siku ya uteuzi.

Kanuni ya 39. - (1) ya tangazo la serikali namba 402 inasema kwamba pingamizi juu ya uteuzi wa mgombea urais au makamu wa rais inaweza kuwasilishwa na mgombea mwingine, mkurugenzi wa uchaguzi, msajili wa vyama vya siasa au mwanasheria mkuu wa serikali.

(3) Pingamizi lililotolewa na msajili wa vyama vya siasa litategemea tu sheria ya gharama za uchaguzi na litakuwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa chini ya sheria na kanuni.

(4) kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mtu mwingine isipokuwa msajili wa vyama vya siasa anayepinga uteuzi wa mgombea yeyote wa urais au makamu wa rais atatoa pingamizi lake kwa tume baada ya kuonyesha fomu za uteuzi, lakini sio zaidi ya saa kumi alasiri ya siku inayofuata siku ya uteuzi.

(5) Pingamizi litawasilishwa kwa tume katika fomu na. 9a kama ilivyoainishwa katika jedwali la kwanza la kanuni hizi.

(6) Uamuzi wa tume chini ya kanuni ndogo ya (6) utakuwa wa mwisho na hautapingwa na mahakama yoyote ya sheria.

(7) Iwapo tume imekubali pingamizi dhidi ya mgombea, itafuta jina la mgombea huyo kwenye orodha ya wagombea walioteuliwa.

### 3.2.4. Rufaa

Mgombea yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi anaweza kukata rufaa kwa tume na uamuzi wa tume utakuwa wa mwisho na hatapingwa katika mahakama yoyote, isipokuwa kwa njia ya shauri la uchaguzi lililowasilishwa kulingana na masharti ya sura ya VII kwa sababu moja au zaidi zilizoainishwa katika sura hiyo [sehemu ya 40 (6) ya sura. 343].

Kanuni ya 31(1) ya tangazo la serikali 402 inasema, mtu asiyeridhishwa na maamuzi ya msimamizi wa uchaguzi chini ya kanuni ya 30(5) anaweza kukata rufaa kwa tume ndani ya saa 24 kuanzia mda maamuzi yalivyotolewa au mda wowote ule kadri tume itakavyoamua.

Kanuni ya 32 - (1) ya tangazo la serikali 402 - Tume inaweza, kabla ya uamuzi wa rufaa, kumwita mtu yeyote kutoa ushahidi au kutoa habari au ufafanuzi kuhusu rufaa.

### 3.2.5. Pingamizi kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa na kukata rufaa kwa pingamizi

Angalia kanuni ya 33 ya tangazo la serikali 402 pia kanuni ya 31 ya tangazo la serikali 401

Kanuni ya 33 - (1) ya gazeti la serikali 402 - Pale ambapo chama cha siasa au mgombea atashindwa kufuata masharti ya kifungu cha 9 na 20 cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi, msajili wa vyama vya siasa ambapo pingamizi linahusu mgombea wa Ubunge anaweza kuweka pingamizi kwa msimamizi wa uchaguzi.

(2) Utaratibu utakaofuatwa katika uamuzi wa pingamizi uliotolewa na msajili na rufaa zozote zitakazofuata baadaye zitakuwa ni taratibu

zilizoainishwa katika kanuni za 31 na 32, isipokuwa kwamba pingamizi la Msajili litatolewa kabla ya siku kumi na nne baada ya siku ya uteuzi.

## 3.3. Kushughulikia Mashauri ya Baada ya Uchaguzi.

Sheria ya uchaguzi nchini Tanzania imeweka njia ya kimahakama katika kusuluhisha migogoro itokanayo na uchaguzi baada ya uchaguzi kukamilika, njia ambayo inaweza kuwa na matokeo ya kubatilisha au kuthibitisha matokeo ya uchaguzi. Pingamizi la madai ya kabla ya uchaguzi imetajwa katika ibara ya 83(1) ya katiba na kifungu cha 108(2) na 107(2) ya sura 343 na sura 292.

Falsafa ya madai ya baada ya uchaguzi inategemea kanuni mbili zifuatazo:

1) Udharura usio na pingamizi na wa haraka wa mchakato mzima wa uchaguzi bila usumbufu kwa njia ya mashauri ya kisheria yanayopinga hatua kati ya kuanza na kumalizika;

2) Utoaji wa mamlaka maalum ambayo yanaweza kuombwa na mtu asiyekubaliana na matokeo au mchakato wa uchaguzi mwishoni mwa uchaguzi, haujumuishi haki na suluhisho kama zao la sheria na zinazodhibitiwa na Katiba.

Kama kanuni ya jumla na bila ubaguzi wowote, katika matokeo ya uchaguzi ya Tanzania yanaweza kuhojiwa tu kupitia shauri la uchaguzi, ambalo linaweza kuwasilishwa katika Mahakama kuu, kupinga matokeo ya uchaguzi wa bunge au katika mahakama za hakimu mkazi au mahakama ya wilaya kwa uchaguzi wa madiwani.

Sheria zinatoa msimamo mpana wa kuleta shauri la uchaguzi chini ya kifungu cha 111 (1) (a) - (d) cha Sura ya 343 & kifungu cha 110 (1) (a) - (d) ya Sura ya 292, ambayo inajumuisha mtu ambaye alipiga kura halali au alikuwa na haki ya kupiga kura kwenye uchaguzi

ambao ombi la uchaguzi linahusiana.

Kuwasilisha shauri kunaambatana na malipo ya shilingi milioni tano za Tanzania (Tshs, 5,000,000 /=) kinachotakiwa kulipwa na muwasilishaji wa shauri kama usalama wa gharama kwa mlalamikiwa, hii ni kwa uchaguzi wa wabunge. Kwa madiwani ni malipo ya laki tano (Tshs. 500,000 /=). Sheria inaruhusu maombi ya kupunguzwa au msamaha kamili wa usalama wa gharama hizi.

Shauri la kupinga matokeo ya uchaguzi wa bunge linapaswa kuletwa ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi na msimamizi wa uchaguzi [kifungu cha 115 - Sura. 343]; na shauri la uchaguzi la kupinga matokeo ya uchaguzi wa madiwani lazima liletwe ndani ya mwezi mmoja tangu tarehe ya kutangazwa kwa matokeo na msimamizi wa uchaguzi [kifungu cha 115 - Sura. 292].

Sheria imeoa mamlaka kwa Mahakama Kuu kusikiliza na kuamua kila shauri la uchaguzi ndani ya miezi kumi na mbili tangu tarehe ya kuwasilisha shauri; na mahakama ndogo chini ya miezi kumi na nane. Hata hivyo, kuna uwezekano wa kuongezewa muda wa kusikiliza na kuamua mashauri ya uchaguzi kwa mujibu wa sheria.

Shauri la kupinga matokeo ya uchaguzi linapaswa kuwa na sababu za msingi ambazo zimeelezewa wazi katika sheria. Sababu hizi zinaweza kujumuisha miongoni mwa zingine, madai ya matumizi ya lugha ya matusi na taarifa za kukashifu wakati wa kampeni au mgombea aliyechaguliwa hakustahili kugombea, hakuteuliwa kihalali au madai ya utumiaji wa vitendo vya rushwa au vitendo visivyoruhusiwa.

Baada ya kupokea ushahidi ambao lazima uthibitishwe kwa kuridhisha mahakama bila shaka yoyote, mahakama inaweza kubatilisha uchaguzi au kuthibitisha mshindi na kisha kutaarifu

mamlaka husika kuhusu maamuzi hayo. Ikiwa mahakama imebatilisha uchaguzi huo basi uchaguzi mdogo inabidi ufanyike kwasababu sheria ya Tanzania hatoi nafasi ya kwa mahakama kutangaza mgombea mwigine kuwa mshindi wa uchaguzi.

Mtu yoyote katika shauri la uchaguzi ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa mahakama ya chini anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwenda mahakama kuu na ikiwa maamuzi yanatoka mahakama kuu moja kwa moja rufaa ni mahakama ya rufaa bila hitaji la kuomba ruhusa ya kukata rufaa katika mahakama kuu.

# Sura ya Nne

## MATUMIZI YA NJIA MBADALA ZA UTATUZI KUTATUA MIGOGORO YA UCHAGUZI

Utaratibu wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi hauweki wazi matumizi ya mifumo ya njia hizi katika kutatua migogoro ya uchaguzi. Ikiwa itazingatiwa katika muktadha mdogo wa sheria za Tanzania, matumizi yanaweza kuwa madogo. Hata hivyo haimaanishi kwamba njia hizi haziwezi kutumiwa katika kutatua migogoro ya uchaguzi.

Kwa kadri sheria ya uchaguzi isivyofafanua kwa kina njia itakayotumiwa katika kutatua migogoro ya uchaguzi, kuna hatua kadhaa za utatuzi ambapo ndani yake njia mbadala za utatuzi zinaweza kutumika.

Mfano sheria ya vyama vya siasa inahitaji kila chama cha siasa, kabla ya kusajiliwa na msajili wa vyama vya siasa, kufafanua kwa kina katika katiba yao utaratibu wa ndani wa utatuzi wa migogoro. Hii inatoa fursa kwa vyama vya siasa vilivyosajiliwa kihalali kutatua migogoro ya vyama kwa kutumia njia mbadala kwa kiwango fulani inaweza pia kutumiwa kutatua malalamiko ya uteuzi wa chama.

Njia mbadala inaruhusu watu na mashirika, pamoja na vyama vya kisiasa na wagombea, kufikia makubaliano kulingana na masilahi yao. Inaweza kuwa isiyo rasmi, kama vile kwenye mikutano na mpatanishi, au michakato rasmi kama usuluhishi ambao maamuzi ya kisheria hufanywa. Aina ya utatuzi wa migogoro inayotumika katika migogoro ya uchaguzi inategemea maslahi na malengo ya vyama vinavyohusika. Njia mbadala inaweza kuruhusu vyama vya siasa, wagombea, wapiga kura, asasi za kiraia na watu binafsi kuwa sehemu ya mchakato wa kiutawala wa kusuluhisha migogoro, kabla, wakati wa uchaguzi na wakati mashauri ya

uchaguzi yamefikishwa mahakamani baada ya uchaguzi. Hii inafanywa kwa kuleta wadaawa pamoja ili kuchunguza na kutatua masilahi yao. Kwa njia hii vyama vinaweza kufuata matokeo ya "shinda-shinda". Kwa hivyo, njia hizi hutoa njia ya kusuluhisha migogoro mingi kwa haraka na kwa ufanisi. Njia hii pia inakuza na kuimarisha maadili ya kidemokrasia kupitia utatuzi wa amani wa migogoro.

### 4.1. Njia za Mbadala za Utatuzi ni nini?

Ni njia ya hiari kwa wahusika kushiriki katika majadiliano ya kujenga, yanayotegemea maslahi, ambayo huanza bila kuwa rasmi hadi taratibu rasmi (kama katika usuluhishi wa kisheria). Lengo ni kukuza maelewano na uhusiano kwa wahusika walio tayari kufikia makubaliano. Aina ya utaratibu mbadala wa utatuzi wa migogoro uliotumiwa katika utatuzi wa migogoro ya uchaguzi utategemea masilahi na vyama husika. Inaweza kutoa njia ya haraka na ya gharama nafuu ya kushughulikia maswala ambayo hayahitaji kushughulikiwa katika mahakama au chombo kingine rasmi cha utatuzi wa migogoro. Walakini, tahadhari lazima ichukuliwe kuhakikisha kuwa haitumiki kama njia ambayo inazuia mchakato rasmi wa kulinda haki za kimsingi za binadamu.

### 4.2. Umuhimu wa Njia Mbadala Katika Utatuzi.

- Utatuzi wa wakati unaofaa: inawezesha utatuzi ndani ya mda mfupi, kwasababu mara moja tu baada ya lalamiko kuletwa linajadiliwa kwa ufupi na haraka huku pande zote mbili zikiwa katika maridhiano.
- Ufikiaji mkubwa wa wahusika: njia hizi zinaweza kutoa ufikiaji mkubwa wa wahusika mfano pale malalamiko yanayotokea wakati uchaguzi ukiendelea na katika vituo vya kupigia Kura, ambapo vyama husika vinapatikana hapo na vina nafasi yakujadili mgogoro wao, kuchunguza na kisha kufikia utatuzi.

- ❖ Majadiliano na ahadi za kurudia: Michakato yake hutoa maazimio yanayofaa zaidi na yanayoweza kudumu kwa vyama.
- ❖ Inatoa fursa ya mazungumzo ya kujenga na/au ahadi za kurudia kati ya wadau walioathirika, ambapo ahadi hizo zinatakiwa au zinahitajika kwa utatuzi endelevu. Matumizi haya ya mwisho yanaweza kuwa muhimu pale ambapo maswala yanahusisha mwenendo chini ya Kanuni za Maadili pia.
- ❖ Marejeo kutoka mahakamani: njia mbadala hukamilisha lengo ya kutatua mgogoro na kutoa mbadala kwa michakato ya kimahakama kwa kutoa njia bora ya kusuluhisha migogoro ambazo matokeo na nia huwa ni "shinda-shinda" (yaani yanatoa ushindi kwa pande zote), kinyume na madai yaendayo mahakama ambapo matokeo huwa ni "shinda-poteza" (yaani maamuzi ya mahakama yanatoa ushindi kwa upande wa mmoja na kupoteza kwa upande mwingine).
- ❖ Imani na Uhalali wa Uchaguzi kuongezeka: mchakato huu unaweza kuongeza hatua za kujenga imani ambayo inaboresha uaminifu wa mchakato wa uchaguzi.

### 4.3. Matumizi ya Njia za Mbadala katika Utatuzi

Njia zote zinategemea "utawala wa sheria". Ili kufikia lengo hili, mchakato wa huu una:

(i) Lazima kuwe na uwazi, hata pale ambapo mazungumzo halisi ya vyama yanaweza kuwa ya siri; na

(ii) Lazima itoe suluhisho kwa wakati unaofaa.

Njia mbadala hufaa katika pande nyingi za mchakato wa uchaguzi ambapo kuna uwezekano wa mgogoro kutokea, na pia ambapo kuna haja ya uamuzi wa haraka ambao utakubalika kwa pande zote. Mifano zingine ni:

- Azimio juu ya kutambuliwa kwa wagombea ambapo kuna haja ya vyama vyenye nia kufikia makubaliano haswa katika uteuzi

ndani ya chama;

- Utatuzi wa migogoro ya ndani ya chama chini ya katiba au kanuni za chama cha siasa;
- Utatuzi wa vizuizi katika usajili wa wapiga kura na kunyimwa haki za kupiga kura;
- Mchakato unaweza kusaidia kusuluhisha kesi mbele ya mahakama, pamoja na kuunda makubaliano juu ya viwango ambavyo vitatumika kuamua masuala na njia zitakazotumiwa kuhakikisha kuwa matokeo yanawakilisha uchaguzi wa chama au kura zilizopigwa siku ya uchaguzi na ni halali.

### 4.4. Matumizi ya Upatanishi katika Kutatua Migogoro ya Baada ya Uchaguzi

Upatanishi ni mchakato ambao mtu wa tatu asiyefungamana na upande wowote huleta pande zinazopingana pamoja katika jaribio la kutengeneza suluhisho linalokubalika kwa njia ya kuwezesha au ya kutathmini na mpatanishi.

Upatanishi kwa kawaida kuhusisha mchakato wa hatua 5 ambazo ni; kukutana kwa pande mbili katika mgogoro, uwasilishaji wa masilahi na malengo yao, mikutano ili kutatua sintofahamu, maoni ya maazimio tofauti na utatuzi wa mwisho wa mgogoro. Katika upatanishi, vyama vinadhibiti mchakato na jukumu la mpatanishi ni kuwaongoza kuelekea suluhisho.

Upatanishi unaweza kufanya kazi katika awamu tatu tofauti;

A. Kuzuia migogoro ya uchaguzi. Mazungumzo ya kisiasa yanaweza kusaidia kuandaa mazingira ya uchaguzi wa amani kupitia kujenga mazingira ya kijamii yenye kuleta mafinikio katika uchaguzi, kuondoa vikwazo na kupunguza uwezekano wa vurugu na matokeo ambayo yanaonekana kuwa haramu.

B. Upunguzaji wa migogoro mikubwa ya uchaguzi na vurugu. Upatanishi unaweza kuwa muhimu kwa mgogoro wa uchaguzi ikiwa mvutano ni mkubwa na ikiwa vurugu zitatokea.

C. Ufuatiliaji baada ya uchaguzi. Upatanishi na mazungumzo ni nyenzo muhimu katika kipindi cha baada ya uchaguzi, ikiwa matokeo ya uchaguzi yatapingwa, lakini pia kushughulikia mvutano na malalamiko yaliyobaki na kuimarisha imani katika mchakato wa kidemokrasia.

# Sura ya Tano

## HITIMISHO LA UJUMLA

Mafanikio katika uchaguzi haimaanishi kufikiwa au kukamilika kwa lengo kuu. Bali, uchaguzi unatakiwa kutizamwa kama njia ya kufikia matarajio makubwa ya utawala bora kupitia raia katika jamii ya kidemokrasia au katika mazingira ya kidemokrasia. Uchaguzi unapaswa kutazamwa kama hatua muhimu katika mwendelezo wa mwingiliano wa kisiasa na kijamii kati ya raia na viongozi katika nchi, ambapo mazungumzo huwa endelevu na mikataba ya kijamii hufanywa upya mara kwa mara na sio kuchukuliwa kama zoezi la kiufundi linalofanyika siku ya uchaguzi tu**.**

Ili kuwepo uzingatiaji wa sheria za utawala wa kisiasa ambao unajenga uchaguzi wa kuaminika na ushindani panahitajika ahadi ya lazima ya vyama vya siasa kuimaraisha demokrasia ya ndani yao. Pale muundo wa ndani wa vyama unapokuwa ni wa usawa basi demokrasia huimarika sana.

Vyama vya siasa vinapaswa na vinaweza kupitisha makubaliano ndani ya katiba zao namna ya kutumia njia mbadala katika kutatua migogoro. Sheria ya Vyama vya Siasa ya 2019 inahitaji vyama vyote vya siasa kupitisha katika katiba zao utaratibu wa kusuluhisha migogoro ndani ya vyama. Lugha ifuatayo inaweza kuzingatiwa katika kuunda mfumo wa utatuzi wa migogoro ndani ya vyama:

"Utangulizi wa katiba: kama chama, tunakubali kusuluhisha migogoro yote ndani ya chama kwa njia ya haki, ya uwazi na ya haraka kupitia upatanishi na njia zingine zinazotambulika za migogoro ya uchaguzi ambayo inawapa wanachama wote haki ya kutangaza masilahi yao na kuzingatia kikamilifu chama kusimamia katiba, sheria za uchaguzi na

jukumu la chama kuimarisha demokrasia na kuhakikisha kuwa migogoro yote inayoweza kusuluhishwa inasuluhishwa kwa amani.

Chama kitashughulikia malalamiko yote, nidhamu ya mwanachama na wafanyakazi, kutokukubaliana na rufaa chini ya katiba ya chama, sheria ndogo ndogo, kanuni na mengineyo kama haya, ya kabla na baada ya uchaguzi na wakati wa uchaguzi kwa haki, haraka na kwa kufuata kikamilifu utaratibu unaotambuliwa na Tume ya taifa ya uchaguzi au mifumo mingine kama hiyo inayotumia pande tatu kuhakikisha kwamba demokrasia inaimarishwa, haki za watu wote kuchaguliwa zinalindwa na migogoro inayoweza kusuluhishwa kwa amani."

## Kiambatanisho I: Uchambuzi wa Malamiko na Migogoro ya Uchaguzi Tanzania

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msimamo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kusimamishwa au kufutwa kwa usajili wa vyama vya siasa** | Kushindwa kufuata masharti ya sheria ya vyama vya siasa mfano chama kutetea ukabila dini, kuvunja katiba, matumizi ya nguvu na vurugu; matumizi ya maneno ya kuchochea, lugha chafu, kf 19 (1) ya SVS | Msajili wa Vyama vya Siasa. Kf 19 (1) SVS | Msajili wa vyama vya siasa. Kf 19 (1) SVS | Haijatajwa | Haijatajwa | Haijatajwa, ila msajili anaweza kuchukua hatua na ufanya uamuzi katika kipindi cha miezi 12 kabla ya uchaguzi. Kf 19 (3) SVA | Hakuna kukata rufaa, maamuzi ni ya Msajili ni ya mwisho. Kf 20 (1) SVS | - | Mapitio ya mahakama |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msimamo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Malalamiko juu ya usajili wa wapiga kura** | Kukataa ombi la kusajiliwa kama mpiga kura, au kutostahiki kusajili<br><br>kf 11 (1), kf 11 (3), kf 21 (1) STU<br><br>Pingamizi juu ya uhifadhi wa majina katika daftari la muda la wapiga kura kf 24 (1) na 24 (2) STU | Afisa usajili kf 21 STU | Mwombaji wa usajili tu anayeomba sababu za kutostahiki<br><br>kf 21 (1) STU<br><br>Pingamizi linalofanywa na mtu yeyote katika daftari la muda la wapiga kura kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi au Afisa wa Usajili kf 24 (1) STU | | Malalamiko chini ya kf 21 hakuna malipo<br><br>Kiasi cha amana kwenye rufaa iliyowekwa na Tume kupitia gazeti la serikali kf 28 (1)<br><br>Mapingamizi chini ya kf 24 (1) hulipiwa kulingana na Tume itakavyotangaza kwenye gazeti kf 25 (2) STU | -<br><br>Uamuzi wa Afisa wa Usajili unapaswa kutolewa ndani ya siku 7 kutoka siku ya mwisho ya kutolewa kwa uchunguzi<br><br>Sehemu ya 26 (7) NEA | Mahakama ya wilaya, kf 21 (2) STU<br><br>Mahakama ya wilaya 27 (1) STU | Siku 14 kuanzia siku ya uamuzi wa afisa msajili kf 21 (1) STU<br><br>Siku 14 kuanzia siku shauri lilipofunguliwa kf 21 (2) STU | Kuhifadhi au usajili wa majina katika sajili ya muda ya wapiga kura, au marekebisho ya daftari la muda la wapiga kura kifungu cha 26 (4) STU<br><br>kuagiza kwamba kadi ya mpiga kura itolewe kwa mwombaji<br><br>Fidia ya fedha kwa mtu ambaye pingamizi limetolewa ikiwa bila sababu ya msingi kifungu cha 26 (5) STU |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msima-mo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Kiasi cha amana kwenye rufaa kwa Mahakama ya Wilaya il-iyowekwa na NEC kupitia gazeti la serikali kf 28 (1) STU | | | | Kuagiza kwamba kitambu-lisho cha mpiga kura kiwasilishwe NEC<br>kifungu cha 29 (2) (a) NEA |
| **Migogoro ya ndani ya chama juu ya uteuzi wa wagombea** | Migogoro dhidi ya utekelezaji wa sheria ndogo za chama hususan uteuzi wa mgombea | Utarat-ibu wa ndani wa utatuzi wa migogoro kf 8D (1) SVS | | | | | | | |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msimamo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Migogoro ya ndani ya chama juu ya taratibu za ki uchaguzi** | Migogoro kati ya vyama haijawekwa wazi katika sheria, hata hivyo malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa msajili wa vyama vya siasa juu ya ukiukaji wa Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa<br>Kanuni. 12 (1) (a) ya Maadili ya Vyama vya Siasa. | Msajili wa vyama vya siasa Kanuni. 12 (1) (b) ya Maadili ya Vyama vya Siasa. | Mtu yoyote, ukijumuisha wanachama wa vyama vya siasa na msajili | Siku 7 kuanzia tarehe ya tukio | | Kamati itaungana na kufanya uamuzi haraka iwezekanavyo baada ya kupokea malalamiko, utetezi na kujumuisha tena au wakati wa kumalizika kwa kuwasilisha utetezi<br>Kanuni. 12 (1) (g) za Maadili ya Vyama vya Siasa | Mapitio ya Mahakama Kuu<br>Kanuni ya 15 (1) ya Maadili ya Vyama vya Siasa | | Onyo au karipio; amuru mhalifu kukosea au kurekebisha ukiukaji; tangazo kwa umma na onyo kwa umma kwa sehemu ya Kisiasa;<br>Au adhabu zaidi iliyotajwa katika sheria ya vyama vya siasa. kusimamishwa, kufuata hatua za jinai haswa pale ambapo kuna ukiukaji unaoendelea.<br>Kanuni. 13 (1) za Maadili ya Vyama vya Siasa |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msima-mo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kukataa kuidhinisha Waangalizi**<br><br>**au kutosta-hiki kwa waangalizi** | Kukataa kwa Tume kuidhinisha waangalizi<br><br>Kanuni ya 18 (5) & (7) ya kanuni za taifa za uchaguzi<br><br>Msimamizi aliyeidhin-ishwa anaweza kukataliwa kwa sababu zifuatazo: | Tume | Tume ina mamlaka ya kukataa idhini kwa waangalizi<br><br>Kanuni. 18 (7) ya Kanuni za uchaguzi | | | | | | |

| **Aina ya mgogoro** | **Vigezo/ sababu** | **Mamlaka ya tukio la kwanza** | **Msima-mo wa kisheria** | **Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko** | **Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko** | **Tarehe ya mwisho ya uamuzi** | **Mamlaka ya kukata rufaa** | **Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa** | **Maamuzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ukiukaji wa sheria za uchaguzi au sheria nyingine yoyote iliyoandik-wa;<br>Ukiukaji wa sheria za uhamiaji;<br>Ukiukaji wa maagizo ya Tume<br>Kujihusisha na kampeni au upen-deleo kwa mgombea au chama cha siasa;<br>kf 20 (1) STU | | | | | | | | |

| **Aina ya mgogoro** | **Vigezo/ sababu** | **Mamlaka ya tukio la kwanza** | **Msimamo wa kisheria** | **Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko** | **Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko** | **Tarehe ya mwisho ya uamuzi** | **Mamlaka ya kukata rufaa** | **Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa** | **Maamuzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Uteuzi wa mgombea** | Kutostahiki kwa uteuzi kwa kutotii Sheria ya Gharama za Uchaguzi<br><br>kf 38 (2) STU<br><br>pingamizi la kuteuliwa mgombea kwa kuzingatia sababu zifuatazo; | Msimamizi wa Uchaguzi (ikiwa sio mpingaji)<br><br>kf 40 (4) STU<br><br>Tume ikiwa mpingaji ni msimamizi<br><br>Kf 40 (5) STU | Mgombea mwingine jimboni, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Msajili wa Vyama vya Siasa, Msimamizi wa Uchaguzi, au Wakili Mkuu<br><br>kf 40 (3) STU imesomwa na Kanuni ya 30 (1) ya Kanuni za Uchaguzi. | Isiwe zaidi ya saa kumi alasiri ya siku inayofuata siku ya uteuzi<br><br>kf 40 (2) Sheria ya Matumizi ya Uchaguzi | | | Rufaa ya kwanza:<br><br>Tume<br><br>Kf 40 (6) STU isomwe na Kanuni ya 31 (1) kanuni za uchaguzi<br><br>Rufaa ya pili:<br><br>Mahakama Kuu kwa njia ya shauri la uchaguzi | Rufaa kwa tume ndani ya saa 24 kutoka maamuzi ya msimamizi yatolewe. Kanuni ya 31 ya kanuni za uchaguzi | Kurejeshwa au kufutwa kwa jina la mgombea husika kutoka kwenye orodha ya wagombea walioteuliwa<br><br>Kanuni. 32 (4) |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msimamo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | maelezo hayatoshi; kushindwa kufuata mahitaji ya STU mgombea hana sifa; kushindwa kufuata sheria ya gharama za uchaguzi<br><br>Kf 40 (1) STU | | | | | | Sehemu ya 40 (6), 110, 111 na 112 ya STU inasomwa na Kanuni. 32 (6) ya Kanuni za uchaguzi | | |
| **Malalamiko yanayohusiana na Kampeni** | **Vitendo vya vyama na wagombea**<br><br>Kushindwa kufuata utaratibu wa ucha | Kamati za Maadili katika Kata, Jimbo, ngazi ya Kitaifa na Kamati ya Rufaa | Mgombea yeyote, Tume, Serikali au chama chochote cha siasa ambacho | Masaa 72 kuanzia mda wa tukio | | Kamati ya maadili inakaa ndani ya masaa 48, inaelekeza utetezi utolewe kwa maandishi | **Rufaa ya Kwanza**:<br><br>Kamati ya Maadili katika ngazi ya juu, | **Uamuzi wa Kamati ya Kata** - kukata rufaa kwa Kamati ya Jimbo kati ya masaa 24 | Kamati ya Maadili inaweza kutoa onyo kwa maneno au kwa maandishi; kuagiza marekebisho ya kosa; tangazo la umma la |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msimamo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | guzi, kusababisha vurugu na usumbufu, matumizi ya lugha mbaya, kutoa tuhuma zisizo na ushahidi, ubebaji wa silaha, kanuni ya 22 ya maadili | Kanuni 5.2<br>Kanuni 5.9<br>Kanuni 5.1<br>KZM | kimetia saini Kanuni.<br>Kanuni 5.4 KZM | | | ndani ya masaa 48, hufanya usikilizaji na kutoa uamuzi ndani ya masaa 48 baada ya vikao vya usikilizaji.<br>Kanuni 5.7 KZM | Kanuni 5.8<br>**Rufaa ya Pili:**<br>Maombi kwa Mahakama Kuu<br>Kanuni 5.8 (g); 5.9 (c); 5.10 (b) | Kanuni 5.8 (a)<br>**Uamuzi wa Kamati ya Jimbo** - kukata rufaa kwa Kamati ya Kitaifa ndani ya masaa 48<br>Kanuni 5.8 (c) | chama kinachoshindwa au mgombea; kukataza chama au mgombea kuendelea na kampeni; kukataza chama au mgombea kusambaza mabango; malipo ya faini ambayo ni kati ya TZS 200,000 hadi TZS 1,500,000 / - |
| | **Vitendo vya tume na wasimamizi** Upendeleo, kubadilisha mipango ya kampeni na Kuchelewesha kutangaza | | | | | **Uamuzi wa Kamati ya Kitaifa** - Kamati ya Rufaa ndani ya masaa 48.<br>Kanuni 5.8 (e) KZM | | | Kanuni 5.11 na 5.12 KZM |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msimamo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | matokeo bila sababu za msingi Kanuni 4.2<br><br>**Vitendo vya Serikali:** Matumizi mabaya ya mamlaka kwa viongozi wa serikali; kutumia rasilimali za serikali kufanya kampeni; Kuzuia au kuvuruga hafla za umma zilizofanyika kulingana na mpango wa kampeni ulioratibiwa; | | | | | | | | |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msima-mo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kuruhusu vyom-bo vya usalama kukandam-iza vyama vya siasa, wagombea au wafuasi;<br><br>Kanuni ya 3.2 ya KZM | | | | | | | | |
| **Malalamiko yanayohusi-ana na upigaji kura** | Kutori-dhika kwa mawakala juu ya maandalizi ya upigaji kura<br><br>Kanuni. 52 (2) Kanuni za uchaguzi | Afisa Ki-ongozi au Msaidizi wa Upigaji Kura<br><br>Kanuni. 62 (2) | mgombea au wakala<br><br>Kanuni. 62 (1) kanuni za uchaguzi | Mara moja katika kituo cha kupigia kura<br><br>Kanuni. 62 (1) kanuni za uchaguzi | | | Rufaa:<br><br>Uamuzi juu ya kuhesabu kura, rufaa iko kwa msi-mamizi<br><br>kf 79 STU | | Kurudia kuhesabu kura kf 78 (1) STU |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msimamo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kutoridhika kwa mpigakura kwenye mchakato wa kupiga kura<br><br>Kanuni. 53 (1) kanuni za uchaguzi | Kura zenye mgogoro huamuliwa na kutatuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msaidizi wa Msimamizi<br><br>Kanuni. 65 (1) | Wagombea au Mawakala wa Vyama vya Siasa kanuni 65 (1) ya kanuni za uchaguzi | Kura zenye utata zinapaswa kuamuliwa mara moja kabla ya kuongezwa kwa kura<br><br>Kanuni. 65 (1) kanuni za uchaguzi | | | shauri la uchaguzi dhidi ya msimamizi wa uchaguzi linaweza kuwasilishwa katika Mahakama Kuu<br><br>kf 79 STU | | |
| **Malalamiko juu ya gharama za uchaguzi** | Kutokuweka wazi kiasi cha fedha kwa mgombea au chama cha siasa kf 20 SGU | Msajili wa vyama vya siasa. Kf 20 (2) SGU. Kanuni ya 18 (1) ya kanuni za gharama ya uchaguzi | Mwombaji wa kuteuliwa kama mgombea, chama cha siasa, mpiga kura, mtu mwingine yeyote<br><br>Kanuni. | | | Uamuzi wa Msajili ndani ya siku 5 baada ya kuwasilisha malalamiko na uamuzi kuuwasilisha kwa | Kwa maombi mahakama kuu. Kf 20 (4) SGU | | Kuondolewa kwa mgombea kushiriki katika mchakato wa uteuzi au uchaguzi. |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msimamo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Maadili yasiyofaa k.m. vitendo vya rushwa kushawishi wapiga kura, wateule, au wakati wa kampeni. kf 21 SGU<br>Fedha zisizofahamika. kf 22 SGU | | 18 (2) kanuni za gharama za uchaguzi<br><br>msajili-anaweza kutoa pingamizi na Mkurugenzi wa Uchaguzi kf 20 (2) SGU | | | Mkurugenzi wa Uchaguzi waTume.<br>kf 20 (4) SGU | | | Kf 20 (1) & (3) , 24 (2) SGU<br><br>Kuwajibika kwa makosa ya rushwa chini ya Sheria ya TAKUKURU Kifungu cha 24 (8) |
| | Uwasilishaji wa wapiga kura. Kf 23 SGU<br><br>Kushindwa kutoa mrejesho wa malipo ya gharama za uchaguzi kwa msajili | | Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mgombea, Chama cha Siasa anaweza kuwasilisha ombi katika Mahakama Kuu | | | | | | Mgombea iwapo amechaguliwa au la, anaweza kuondolewa na atatozwa faini ya TZS 2M au kifungo cha mwaka 1 kwa kukosa kutoa mrejesho wa |

| Aina ya mgogoro | Vigezo/ sababu | Mamlaka ya tukio la kwanza | Msima-mo wa kisheria | Tarehe ya mwisho ya kupeleka malalamiko | Kiasi cha fedha cha kufungua malalamiko | Tarehe ya mwisho ya uamuzi | Mamlaka ya kukata rufaa | Tarehe ya mwisho ya kukata rufaa | Maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ndani ya siku 180 baada ya uchaguzi kf 18 (2) SGU<br><br>Kutoa habari za siri Kanuni ya 18 (2) (a) - (e) ya kanuni za gharama za uchaguzi | | | | | | | | malipo ya gharama za uchaguzi. kf 18 (5) SGU<br><br>Chama cha siasa kinaweza kutozwa faini ya TZS 3M au kutostahiki kushiriki n uchaguzi mkuu ujao Sehemu ya 18 (4) SGU |

**SVS- SHERIA YA VYAMA VYA SIASA**
Kf- KIFUNGU
STU- SHERIA YA TAIFA YA UCHAGUZI
ALAMA (-) – SHERIA IKO KIMYA
KZM- KANUNI ZA MAADILI

SGU- SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI

## Kiambatanisho II: Uchambuzi wa Makosa ya Jinai katika Uchaguzi:

| KOSA LA JINAI | VIGEZO VYA KOSA | ADHABU |
|---|---|---|
| Kughushi kwenye daftari la kudumu la wapiga kura.<br><br>Kf. 90 STU | kumiliki, kudhibiti kadi ya mpiga kura ambayo ni ya mtu mwingine | Faini isiyopungua chini ya shilingi laki moja (TZS 100,000) na isiyozidi shilingi laki tatu (TZS 300,000) au kifungo kisichopungua mwaka na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja. |
| uchapishaji wa taarifa ya uongo ya kuondolewa kwa mgombea. kf 91 STU | Uchapishaji wa makusudi, kuchapisha taarifa yoyote ya kuondolewa kwa mgombea kwa madhumuni ya kumtangaza mgombea mwingine | Kifungo kisichozidi miaka miwili |
| Ushawishi wa rushwa ya kujitoa kama mgombea. kf 91B STU | Kushawishi, kushauri mtu mwingine ajiondoe kuwa mgombea kwa kuzingatia malipo | Kifungo kisichozidi miaka 5 |
| Kutoa ushahidi wa uongo / kutoa taarifa ya uongo. kf 92 STU | Kuwasilisha kitambulisho cha uongo katika kuthibitisha utambulisho wa mtu binafsi | Kifungo sio chini ya miezi 6 |
| Kushindwa kudumisha usiri katika uchaguzi. kf 93 STU | -Kupata au kujaribu kupata habari kuhusu kura za watu wengine. Kf 93 (4) STU<br><br>-Kutoa habari yoyote iliyopatikana katika kuhesabu kura. Kf 93 (5) STU | Faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja. kf 93 (7) STU |
| Vitendo vya rushwa. kf 94 STU | Ushawishi usiofaa, hongo kf 94 STU | Faini isiyopungua shilingi laki tano (TZS 500,000) au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka na kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja |

| KOSA LA JINAI | VIGEZO VYA KOSA | ADHABU |
|---|---|---|
| Kujifanya mtu flani. kf 95 | Kuomba karatasi ya kupigia kura kwa jina la mtu mwingine, kf 101 (a)<br><br>kutumia kadi ya mtu mwingine<br><br>Sehemu ya 101 (b) | Faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi laki mbili au kifungo cha chini ya miezi sita na si zaidi ya miezi kumi na mbili. |
| Ushawishi usiofaa kf 99 | Moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kutishia kutumia nguvu, vurugu au kizuizi, kuumiza au kutishia kufanya hivyo, uharibifu, madhara au upotezaji au dhidi ya mpiga kura yeyote ili kumlazimisha mpiga kura kupiga kura au kutokupiga. | - |
| Kuondolewa kwa taarifa. kf 105 | Bila mamlaka halali kuharibu, kuchafua au kuondoa ilani yoyote ambayo imeonyeshwa chini ya Sheria | Faini isiyopungua shilingi elfu thelathini na sio zaidi ya shilingi laki moja au kifungo jela kwa chini ya mwezi mmoja na sio zaidi ya miezi sita au vyote kwa pamoja. |
| -Mikutano ya hadhara siku ya uchaguzi, kf 104 NEA<br><br>-Kuonyesha nembo ya chama katika maeneo ya karibu na kituo cha kupigia kura. kf 104 | Kufanya mkutano siku ya uchaguzi au ndani ya jengo lolote ambalo upigaji kura katika siku ya uchaguzi au katika eneo la mita 200 au jengo hilo huvaa au kuonyesha picha yoyote ya kadi kwa niaba ya mgombea fulani | Faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki moja. Sehemu ya 104 (2) NEA |

| KOSA LA JINAI | VIGEZO VYA KOSA | ADHABU |
|---|---|---|
| Vitendo visivyo sawa. kf 21 | Kutoa au kukopesha kwa njia isiyo ya moja kwa moja au ya moja kwa moja, kutoa au kuahidi kutoa pesa yoyote au kuzingatia muhimu kwa mpiga kura yeyote ili kushawishi mpiga kura yeyote kupiga kura au kujizuia kupiga kura kf 21 (1) (a) SMU | -Kutostahiki kushiriki uchaguzi. Kf 24 (1) SMU<br>-kuanzisha kesi ya jinai au ombi la uchaguzi dhidi ya mgombea huyo Sehemu ya 24 (3) (4) EEA |
| | Kutoa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja au kununua au kujaribu kupata, ofisi yoyote, mahali au ajira, kwa mpiga kura yeyote,<br>Kf 21 (1) (b) SMU | - Kutostahiki kushiriki uchaguzi. Sehemu ya 24 (1) SMU<br>- kuanzisha kesi ya jinai au ombi la uchaguzi dhidi ya mgombea huyo kf 24 (3) & (4) SMU |
| | Kutoa zawadi, mikopo, ofa, ahadi, manunuzi au makubaliano kwa lengo la kushawishi mtu fulani kuchaguliwa awe mbunge, diwani au raisi au ili mtu fulani ateuliwe kua mgombea wa nafasi yoyote, kf 21 (1)(c) SMU | - Kutostahiki kushiriki uchaguzi kf 24 (1) SMU<br>- kuanzisha kesi ya jinai au ombi la uchaguzi dhidi ya mgombea huyo KF 24 (3) & (4) SMU |
| Hongo kf 21 (1) (e) | Kulipa au kusababisha hongo kulipwa kwa mtu katika mchakato wa uteuzi | - Kutostahiki kushiriki uchaguzi. kf 24 (1) SMU<br>- Mashauri ya jinai au ombi la uchaguzi dhidi ya mgombea huyo, kf 24 (3) & (4) SMU |

| KOSA LA JINAI | VIGEZO VYA KOSA | ADHABU |
|---|---|---|
| | Kupokea au kukubaliana malipo ya kiasi chochote cha fedha ili kumpigia kura mgombea fulani | - Kutostahiki kushiriki uchaguzi. kf 24 (1) SMU<br>- Mashauri ya jinai au ombi la uchaguzi dhidi ya mgombea huyo, kf 24 (3) & (4) SMU |
| Mapato yasiyo na chanzo. kf 22 (a) (f) SMU | kutoa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, au kutoa, au kulipa, kabisa au kwa sehemu, gharama ya kutoa au kutoa chakula, kinywaji, burudani au masharti kwa au kwa mtu yeyote, kwa kusudi la kumshawishi mtu huyo, au mtu mwingine yeyote, kupiga kura au kujiepusha na upigaji kura katika mchakato huo wa uteuzi au uchaguzi | - Kutostahiki kushiriki uchaguzi.<br>Kf (1) SMU<br>- kuanzisha kesi ya jinai au ombi la uchaguzi dhidi ya mgombea huyo kf 24 (3) & (4) SMU |

| KOSA LA JINAI | VIGEZO VYA KOSA | ADHABU |
|---|---|---|
| Makosa yanayohusiana na ofisi ya msajili. kf 27 SMU | Kuzuia Msajili au mwakilishi wake kutumia mamlaka ya Msajili chini ya Kifungu cha 27 (a) SMU<br><br>Kukataa kutoa vitabu, karatasi na nyaraka kama inavyoombwa na Msajili kf 27 (b) SMU<br><br>Kuzalisha vitabu vya uwongo, nyaraka au habari za uwongo kwa Msajili Sehemu ya 27 (c) SMU<br><br>Kutoa taarifa ya uwongo katika mapato yoyote au ripoti ya kifedha Sehemu ya 27 (d) SMU<br><br>Kuondoa vitabu, karatasi, nyaraka au kitu chochote kinachohusiana na maswala ya uchunguzi, uchunguzi au ukaguzi kf 27 (e) SMU. | |
| Uvunjaji wa sheria za uchaguzi, kanuni ya 13<br><br>(Maadili ya Vyombo vya Habari ya Utangazaji wa Uchaguzi Tanzania 2015) | Kitendo chochote kinyume na sheria za uchaguzi kama kanuni ya 16 (1) ya Kanuni za Utangazaji (Maudhui) | -Kufungiwa kwa chombo cha habari<br><br>-Kufunguliwa mashtaka ya jinai. |

**STU- Sheria ya Taifa ya Uchaguzi**
Kf- kifungu
SMU- Sheria ya Matumizi ya Uchaguzi